JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SABA

04 NOVEMBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA SABA – TAREHE 04 NOVEMBA, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

96. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga jengo la ICU katika Hospitali ya Wilaya ya Urambo.

97. MHESHIMIWA DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (KISARAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kiluvya kwa Komba hadi Kituo cha Afya na kwa Sumaye hadi Majumba Sita kwa kiwango cha lami.

98. MHESHIMIWA ENG. AMOSY WILLIAM MAGANGA (SIKONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la kisasa katika Mji wa Sikonge.

99. MHESHIMIWA MABULA JOHNSON MAGANGILA (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara za Mitaa katika Kata za Isaka, Segese, Bulyankulu na Bulige kwa kiwango cha lami.

100. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Barabara ya Mbulu – Masieda – Mang'ola – Karatu ili kurahisisha usafiri wa kwenda Bariadi kutoka Mbulu Mjini.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

101. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Walimu walioajiriwa Mwaka 2009 ambao wamekidhi vigezo watapandishwa Madaraja wanayostahili na kulipwa malimbikizo yao.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

102. MHESHIMIWA YUMNA MMANGA OMAR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, hatua gani zimechukuliwa kwa Watu Wenye Ulemavu kupata fursa za kiuchumi za uhifadhi mazingira, usimamizi wa taka na Uchumi wa Kijani.

WIZARA YA MAJI:

103. MHESHIMIWA JOSHUA SAMWEL NASSARI (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji ya Uwiro, Imbaseni, Kikatiti na Samaria.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

104. MHESHIMIWA OTHMAN MAULID SULEIMAN (MAHONDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usalama wa Madereva Bodaboda na Pikipiki zao kutokana na matukio ya kudhulumiwa na kuibiwa.

105. MHESHIMIWA ASHA JUMA FERUZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Kata ya Vijibweni Wilaya ya Kigamboni.

WIZARA YA KILIMO:

106. MHESHIMIWA ASHA SALUM MOTTO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuinua Kilimo cha Umwagiliaji Mkoani Mtwara.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

107. MHESHIMIWA MARIAM ANZURUNI MUNGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini utungaji wa Sera ya Nyumba (*Housing Policy*) na Sheria ya Nyumba (*Housing Act*) utakamilika ili sekta hii ipate usimamizi wa Kisheria.

WIZARA YA UJENZI:

108. MHESHIMIWA KHALID MUSSA NSEKELA (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Km 50 kutoka Rwenkorongo – Nkwenda hadi Omurushaka utakamilika.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

109. MHESHIMIWA SELINA HENRY KINGALAME (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya Wahadhiri na kuboresha maslahi yao ili kuimarisha ubora wa ufundishaji.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

110. MHESHIMIWA ARIF SULEIMAN PREMJI (MTWARA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Kiwanda cha Mbolea kitajengwa katika Jimbo la Mtwara Vijijini kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Mwaka 2025 – 2030.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

111. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMAN BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama katika Tarafa zilizopo maeneo ya Milimani Same.

112. MHESHIMIWA MECKTRIDIS FRATERN MDAKU (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya – Malinyi ili kurahisisha upatikanaji wa Haki kwa Wananchi.

III. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa

Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 na tarehe 30 Juni, 2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC):

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
04 NOVEMBA, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE